# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

# 2013/14

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2013

## Utangulizi

Tamko la Sera ya Fedha hutolewa na Benki Kuu kwa mujibu wa sheria linaloweka bayana malengo ya sera ya fedha, msingi wa malengo hayo na hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa kufikia malengo hayo. Tamko hili kwa mwaka 2013/14 linajumuisha mapitio ya utekelezaji wa sera ya fedha ya mwaka 2012/13 na kuainisha malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2013/14.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Katika kipindi cha mwaka 2012, uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 4.0 kwa mwaka 2011. Kati ya mwaka 2011 na 2012, ukuaji wa pato halisi kwa mataifa yaliyoendelea *(advanced economies)* ulipungua kutoka asilimia 1.6 hadi asilimia 1.2. Ukuaji wa pato halisi kwa mataifa yanayoibukia kiuchumi *(emerging market economies)* na yale yanayoendelea kiuchumi (developing economies) ulipungua kutoka asilimia 6.4 hadi kufikia asilimia 5.1 kutokana na kupungua kwa: uwekezaji, matumizi ya bidhaa kwa walaji *(final consumption),* na uzalishaji viwandani. Vivyo hivyo, pato halisi katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara lilikua kwa wastani wa asilimia 4.8 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2011. Kupungua kwa ukuaji huo kulitokana na mafuriko yaliyoikumba Nigeria, migomo ya wafanyakazi nchini Afrika Kusini, kukatizwa kwa mauzo ya nje ya mafuta kutoka Sudani ya Kusini na migogoro iliyoikumba Mali na Guinea Bissau. Kulingana na Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa mwezi Aprili 2013 *(IMF World Economic Outlook, April 2013)*, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2013 na asilimia 4.0 mwaka 2014. Ukuaji huu utachangiwa na utekelezaji wa sera zinazolenga kupunguza madhara yaliyotokana na mtikisiko wa uchumi katika nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya na Marekani.

Kasi ya upandaji wa bei duniani ilipungua mwaka 2012 kutokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa. Kwa mataifa yaliyoendelea, mfumuko wa bei ulipungua kutokana na kushuka kwa bei za nishati. Katika nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea kiuchumi, kushuka kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na kupungua kwa bei za vyakula. Mfumuko wa bei ulipungua Kusini mwa Jangwa la Sahara kutokana na sera za fedha za kudhibiti ujazi wa fedha kwenye uchumi pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula. Taarifa ya Mwelekeo wa Hali

ya Uchumi wa Dunia ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Aprili 2013 inaonesha matarajio ya kupungua zaidi kwa mfumuko wa bei mwaka 2013.

**Mwenendo wa Uchumi Tanzania**

***Tanzania Bara***

Katika mwaka 2012, uchumi uliendelea kuimarika na kukua kwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na lengo la mwaka la ukuaji wa asilimia 6.8, na ukuaji halisi wa asilimia 6.4 uliofikiwa mwaka 2011. Kiwango hiki cha ukuaji wa uchumi kilitokana na hali nzuri ya hewa, usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati uliosaidia kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo; na kuimarika kwa upatikanaji wa umeme ulioongeza uzalishaji wa bidhaa za viwandani. Shughuli nyingine za kiuchumi zilizochangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Pato la Taifa ni pamoja na mawasiliano na biashara.

Kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa inatarajiwa kuongezeka katika mwaka wa fedha 2013/14 kufikia asilimia 7.1 kutokana na uwekezaji unaoendelea kwenye sekta ya miundombinu na matarajio ya hali nzuri ya hewa. Matarajio ni kwamba kuimarika kwa ushirikiano wa jumuiya za kikanda kutaongeza mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi na mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji, na hivyo kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa.

Mfumuko wa bei ulishuka na kufikia kiwango cha tarakimu moja mwezi Machi 2013, baada ya kuwa kwenye tarakimu mbili kwa kipindi cha miezi 21 mfululizo. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulitokana na hali nzuri ya hewa katika ukanda wa Afrika Mashariki iliyopelekea kuongezeka kwa upatikanaji wa chakula pamoja na sera ya kudhibiti ujazi wa fedha. Mfumuko wa jumla wa bei *(headline inflation)* ulipungua hadi kufikia asilimia 9.4 mwishoni mwa mwezi Aprili 2013, ikilinganishwa na asilimia 18.7 mwezi Aprili 2012, wakati mfumuko wa bei za vyakula (food inflation) ulipungua kufikia asilimia 10.2 kutoka asilimia 24.7. Mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati *(core inflation)* ulibakia kwenye tarakimu moja kwa kipindi chote.

Katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013, mapato ya Serikali yalifikia asilimia 92.5 ya lengo. Mapato ya kodi yalifikia asilimia 95.6 ya lengo kutokana na makusanyo mazuri ya kodi ya mapato. Matumizi ya Serikali yalifikia asilimia

85.0 ya makadirio, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa asilimia 88.2. Wakati huo huo, matumizi ya maendeleo yalikuwa asilimia 78.8 ya makadirio kutokana na baadhi ya wahisani kuchelewa kutoa fedha za miradi ya maendeleo pamoja na kuchelewa kupatikana kwa fedha za mikopo ya kibiashara *(external non-concessional loans)*.

Kwa mujibu wa vigezo vinavyotumika kutathmini hali ya mabenki, sekta ya mabenki imeendelea kuimarika. Aidha tathmini ya awali imeonesha kuwa mabenki hayo ni salama na yanaweza kuhimili misukosuko ya kifedha. Takwimu hizo zinaonyesha kuwa mabenki mengi yametimiza masharti mapya ya kuongeza mtaji *(capital requirement)* kutoka shilingi bilioni 5 hadi shilingi bilioni 15 hata kabla ya tarehe ya mwisho ambayo ni Februari 2015. Katika kipindi cha Julai 2012 hadi Aprili 2013, Benki Kuu ilitoa leseni kwa taasisi ndogondogo za fedha mbili ili kuziruhusu kufanya shughuli za kibenki. Vile vile, kufuatia kukamilika kwa mwongozo wa uwakala wa huduma za kibenki *(Guidelines on Agency Banking, February, 2013)*, Benki Kuu ilitoa leseni kwa benki tatu ili kuziruhusu kutoa huduma hizo. Utaratibu huu wa uwakala unapanua wigo wa huduma za kibenki hivyo kuwafikia walengwa wengi zaidi kwa gharama nafuu. Pia mabenki mengi yameendeleza ushirikiano na makampuni ya simu kutoa huduma za kifedha na malipo kupitia simu za mikononi. Kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia yanayoendelea katika sekta ya fedha, Benki Kuu inafanya tathmini ya kanuni mbalimbali na kuangalia haja ya kuwa na sheria mpya ili kuendana na mabadiliko hayo.

Katika kipindi cha miezi kumi ya mwaka wa fedha 2012/13, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali na nchi za nje *(current account deficit)* ilipungua kufikia dola za Kimarekani milioni 3,332.7 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani milioni 3,680.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2011/12. Mwenendo huu ulitokana na uzalishaji mzuri na mauzo ya bidhaa asilia na bidhaa za viwandani pamoja na kupungua kwa uagizaji wa mitambo ya uzalishaji, bidhaa za walaji na malighafi za viwandani.

Kufikia mwishoni mwa Aprili 2013, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Kimarekani milioni 4,384.7 ambazo zinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa wastani wa kipindi cha miezi 4.3. Wakati huo huo, rasilimali za fedha za kigeni za mabenki zilifikia dola za Kimarekani milioni 913.8.

*Zanzibar*

Katika mwaka 2012, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 7.0, ikilinganishwa na matarajio ya ukuaji wa asilimia 7.5 na ukuaji halisi wa asilimia 6.7 mwaka 2011. Ukuaji wa uchumi ulichochewa kwa kiasi kikubwa na ukuaji kwenye sekta za ujenzi, usafirishaji na mawasiliano.

Katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili, 2013 mfumuko wa bei ulibakia kwenye kiwango cha tarakimu moja na kufikia asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 9.9 iliyokuwa imefikiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2012. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na kushuka kwa bei za vyakula, hususan mchele, ngano na sukari.

Katika kipindi cha miezi kumi ya mwaka wa fedha 2012/13, mapato ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 297.6. Mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 222.3, pungufu ya lengo kwa asilimia 6.9. Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 357.8, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 226.2. Matumizi kwa ajili ya shughuli za maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 130.4. Nakisi katika bajeti ya serikali ilifikia shilingi bilioni 52.2 ambayo iligharamiwa na mikopo kutoka nje ya nchi.

Katika kipindi cha miezi kumi ya mwaka wa fedha 2012/13, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani milioni 68.4 ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 67.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2011/12. Hali hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha mauzo *(volume)* na kushuka kwa bei ya karafuu, pamoja na ongezeko kubwa la uagizaji wa bidhaa za chakula na mitambo ya uzalishaji.

**Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2012/13**

***Malengo ya Sera ya Fedha***

Katika mwaka wa fedha 2012/13, Benki Kuu ya Tanzania iliweka malengo yafuatayo ili kufikia malengo ya uchumi mpana ya Serikali:

i. Ukuaji wa wastani wa `fedha taslimu usiozidi asilimia 16.0;
ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 18.0;

iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 20.0; na
iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne na nusu (4.5).

***Utekelezaji wa Sera ya Fedha***

Katika kipindi cha miezi kumi ya mwaka wa fedha 2012/13, Benki Kuu, iliendelea na sera ya kudhibiti ujazi wa fedha ili kushusha matarajio ya mfumuko wa bei.

Ili kufikia malengo hayo, Benki Kuu iliongeza sehemu ya amana za Serikali ambayo mabenki yanatakiwa kuhifadhi Benki Kuu *(reserve requirements)* kutoka shilingi 30 hadi shilingi 40 katika kila shilingi 100. Vile vile Benki Kuu, iliongeza mauzo ya dhamana za Serikali katika soko la fedha *(open market operations)* na mauzo ya fedha za kigeni kwa lengo la kupunguza ukwasi kwenye mzunguko. Kutokana na sera ya kudhibiti ujazi wa fedha, ukuaji wa wastani wa fedha taslimu *(average reserve money)* kwa mwaka unaoishia Machi 2013 ulibaki ndani ya malengo; wakati ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M3) ulikuwa asilimia 15.3 ukilinganisha na makadirio ya asilimia 18.0. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 21.1 ikilinganishwa na makisio ya asilimia 18.2. Katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2013, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ulikua kwa asilimia 16.5 ikilinganishwa na lengo la asilimia 18 kwa mwaka unaoishia Juni 2013. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 20.1 ikilinganishwa na makisio ya asilimia 20 kwa mwaka unaoishia Juni 2013.

Kutokana na mwelekeo wa sera ya fedha, riba katika soko la fedha kati ya mabenki *(interbank cash market*) na ile ya dhamana za serikali *(Treasury bills*) iliongezeka, hali ambayo pia ilijidhihirisha kwenye kupanda kwa riba za amana na mikopo ya mabenki nchini.

Kutokana na utekelezaji huu wa sera ya fedha, vigezo vyote vya mpango wa Policy Support Instrument (PSI) katika kipindi toka Julai 2012 hadi Machi 2013 vilifikiwa isipokuwa kile kinachohusu mikopo ya ndani kwa bajeti ya Serikali *(Net Domestic Financing)* ambacho kilivuka ukomo kwa kiasi cha shillingi bilioni 149.7, sawa na asilimia 0.3 ya Pato la Taifa. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa uwiano kati ya mapato na matumizi ya Serikali hali ambayo inatarajiwa kufikiwa ifikapo Juni 2013.

**Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2013/14**

Katika mwaka 2013/14, Serikali itaimarisha ukusanyaji wa mapato, na kuzingatia uwiano wa mapato na matumizi na hivyo kudhibiti ukuaji wa deni la Taifa. Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.1 kutokana na makadirio ya ukuaji wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2013 na asilimia 7.2 kwa mwaka 2014. Juhudi za kudhibiti mfumuko wa bei zitaendelea ili ubaki kwenye kiwango cha tarakimu moja.

Wakati ikiendelea na jitihada za kuimarisha sekta ya fedha ili huduma za kibenki ziweze kuwafikia Watanzania wengi *(unbanked and the under banked population)* na kwa kuzingatia mahitaji ya uchumi mpana, Benki Kuu imepanga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslimu usiozidi asilimia 14.0;
ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 15.0;
iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 19.6; na
iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.0.

Muundo na utekelezaji wa sera ya fedha utaendelea kuzingatia mfumo wa kudhibiti ukuaji wa fedha taslimu *(reserve money programming framewor*k) ukitumia nyenzo mbalimbali za sera zitakazohakikisha kuwa ukwasi unabakia ndani ya malengo. Pamoja na mfumo huo, Benki Kuu inalenga kutumia riba yake *(policy rate)* kama kiashiria cha mwelekeo wa sera ya fedha.

Soko la dhamana za Serikali litaendelea kuwa msingi wa mfumo wa kiwango cha riba kinachotumika katika masoko ya fedha.

Kiwango cha ubadilishanaji wa fedha za kigeni katika soko la jumla la mabenki *(inter-bank foreign exchange market)* kitaendelea kuongozwa na nguvu za soko. Aidha, Benki Kuu itaendelea kushiriki katika soko la fedha za kigeni kwa ajili ya kuhakikisha kiwango cha ujazi wa fedha kinakuwa ndani ya malengo na kupunguza madhara ya mabadiliko makubwa katika kiwango cha ubadilishanaji wa fedha za kigeni. Haya yote yatatekelezwa kwa kuzingatia kwamba kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinabaki ndani ya malengo.

**Hitimisho**

Mkakati wa Benki Kuu wa kudhibiti ujazi wa fedha mwaka 2012/13 umesaidia kushusha mfumuko wa bei hadi kufikia kiwango cha tarakimu moja bila kuathiri ukuaji wa uchumi. Mkakati huu utaendelezwa katika mwaka 2013/14. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 7.1 mwaka 2013/14 ukichochewa na uwekezaji unaoendelea kwenye miundombinu, matarajio ya utulivu wa bei za bidhaa za mafuta katika soko la kimataifa na hali nzuri ya hewa nchini. Juhudi zinazoendelea kuimarisha jumuiya za kikanda zinatoa fursa zaidi za kuongezeka kwa uuzaji bidhaa nje ya nchi pamoja na kuongeza mapato ya huduma za usafirishaji, na hivyo kuchangia ukuaji wa pato la Taifa.

Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuwa makini katika kudhibiti mfumuko wa bei, ikiwa ni pamoja na kupitia upya malengo ya sera ya fedha kama ikibidi kufanya hivyo. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha utulivu kwenye sekta ya fedha na kupanua wigo wa huduma za kifedha ili ziwafikie wananchi wengi zaidi.

Benki Kuu itapitia mikakati mbalimbali inayotumika katika utekelezaji wa sera za fedha ili kuangalia uwezekano wa kutumia riba yake (policy rate) kama kiashiria cha mwelekeo wa sera ya fedha. Serikali inadhamiria kutekeleza sera ambazo zinalenga kuleta matokeo bayana, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba kiwango cha upatikanaji wa chakula kinakuwa cha kutosha. Kutokana na dhamira hii ya Serikali, Benki Kuu ina imani kwamba malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2013/14 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, S.L.P 2939, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233329, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
http://www.bot.go.tz